# UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Toleo Na. 10 | Desemba, 2022




# VYAMA 16 VYASHIRIKI UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE NA UDIWANI

TUFAHAMU TUME

# MZUNGUKO WA UCHAGUZI

*Inaendelea kutoka toleo la Novemba, 2022*

**Uraia wa Tanzania kwa kurithi:**
Mtu yeyote aliyezaliwa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya Muungano au baada ya Muungano atahesabika kuwa raia wa Tanzania kwa kurithi kuanzia tarehe ya kuzaliwa kwake, kama siku ya kuzaliwa kwake mama au baba yake ni raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzaliwa au tajnisi. Hii ina maana kuwa kama wazazi wake walikuwa ni raia wa Tanzania wa kurithi wakati wa kuzaliwa kwake mtu huyo hawezi kuwa raia wa Tanzania wa kurithi.

**Uraia wa Tanzania kwa Tajnisi**
Mtu yeyote ambaye siyo raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa au kurithi anaweza kuomba uraia wa Tanzania wa tajnisi kwa mujibu wa vifungu vya 8 na 9(1) vya Sheria ya Uraia ya mwaka 1995
Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya uraia nchini ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya kutoa au kutotoa Uraia wa Tanzania kwa wageni




# Vyama 16 vyashiriki Uchaguzi Mdogo wa Ubunge na Udiwani

***Na Mwandishi wetu***

Jumla ya vyama vya siasa 16 vimeshiriki uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo la Amani lililopo wilaya ya mjini, mkoa wa Mjini Magharibi, katika kisiwa cha Unguja na uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata 7 za Tanzania Bara.

Uchaguzi huo ambao umefanyika Desemba 17, 2022, ulitoa fursa kwa jumla ya wapiga kura 114,647 katika vituo vya kupigia kura 289 katika jimbo la Amani na kata 7 za Tanzania bara kushiriki uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa msimamizi wa uchaguzi wa jimbo la Amani Safia Iddy, wagombea walioteuliwa kuwania ubunge katika jimbo hilo na vyama vyao kuwa ni pamoja na Hidaya Hassan Ameir wa chama cha Demokrasia Makini, Bashiri Katabu Said wa NLD, Barik Ali Omar

wa UPDP, Mashavu Alawi Haji wa UMD, na Pandu Haji Pandu wa TLP.

Wagombea wengine ni Lela Omar Salim wa chama cha CCK, Abdul Yussuf Maalim wa CCM, Khalfani Kheir Simai wa NRA, Naima Salum Hamad wa chama cha UDP, Azani Awesu Azani wa SAU, John Charles Mboggo wa ADC, Mohammed Khamis Mohammed wa ACT WAZALENDO, Musoma Emanuel Musoma wa DP na Abdi Abdalla Haji wa CUF.

Kwa upande wa uchaguzi wa Madiwani, kabla ya zoezi la uteuzi, jumla ya kata 12 zilitarajiwa kushiriki uchaguzi huo, lakini baada ya zoezi la uteuzi na uamuzi wa rufaa za wagombea udiwani kukamilika, uchaguzi wa udiwani umefanyika katika kata 7 za Tanzania bara.

Wapiga kura walishiriki kupiga kura katika Kata ya Majohe iliyopo Jiji la Dar es Salaam, Kata ya Mndumbwe iliyopo Wilaya ya Tandahimba, kata ya Njombe Mjini katika Mji wa Njombe, Kata ya Dunda katika Wilaya Bagamoyo, na Kata ya Mwamalili katika Manispaa ya Shinyanga

Pia uchaguzi huo umefanyika katika kata ya Mnyanjani katika Jiji la Tanga na Kata ya Vibaoni iliyopo katika Mji wa Handeni.

Kata ambazo hazikufanya uchaguzi baada ya wagombea udiwani katika kata hizo kupita bila kupingwa au baadhi ya wagombea kukosa sifa za uteuzi ni pamoja na kata ya Dabalo katika Wilaya ya Chamwino, kata ya Ibanda katika Wilaya ya Kyela, kata ya Misugusugu katika Mji wa Kibaha na Kata ya Kalumbeleza katika Wilaya ya Sumbawanga.

Kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kampeni za Uchaguzi huo mdogo zilifanyika kuanzia tarehe 1 hadi 16 Desemba, ambapo Tume iliwataka wapiga kura waliopoteza vitambulisho vyao vya mpigakura kutumia vitambulisho mbadala ikiwemo pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kitambulisho cha uraia ili kushiriki zoezi la kupiga kura kwenye uchaguzi huo mdogo.

Hata hivyo taarifa hiyo ilisisitiza kuwa mpiga kura aliyepaswa kutumia kitambulisho mbadala ni yule tu aliyeandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapiga kura na jina lake lipo kwenye kituo husika.

Uchaguzi wa ubunge katika Jimbo la Amani ulifanyika kufuatia aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa kufariki dunia mnamo tarehe 13 Oktoba, 2022, huko mjini Unguja.




# Watendaji wa Uchaguzi waaswa kufanya kazi kwa weledi

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewataka watendaji wa uchaguzi katika Jimbo la Amani Tanzania Zanzibar na kata 12 za Tanzania Bara kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake, Maadili ya Uchaguzi na maelekezo ya Tume.

Wito huo umetolewa hivi karibuni katika mafunzo ya watendaji hao yaliyofanyika Unguja, Morogoro na Iringa ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Amani na kata 12 za Tanzania Bara uliofanyika tarehe 17 Desemba, 2022.

Akizungumza kwenye mafunzo ya Watendaji wa Uchaguzi Unguja,

Mjumbe wa Tume Mhe. Balozi Omari Ramadhani Mapuri amesema sanjari na kuzingatia miongozo hiyo watendaji hao walipaswa kufanya kazi kwa weledi.

Aliongeza kuwa uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali za kufuatwa na kuzingatiwa kwa kuwa hatua na taratibu hizo ndiyo msingi wa uchaguzi mzuri, wenye ufanisi na unaopunguza malalamiko na vurugu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalihusisha mada mbalimbali na majadiliano ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika hatua zote za uchaguzi, hivyo Balozi Mapuri aliwataka wasimamizi wenye uzoefu kutumia mafunzo hayo kujiongezea maarifa mapya na wale wapya kujifunza kwa haraka.

“Nitumie fursa hii kuwaasa kuwa pamoja na uzoefu ambao baadhi yenu mnao katika uendeshaji wa uchaguzi, mhakikishe mnazingatia maelekezo mtakayopewa na Tume badala ya kufanya kazi kwa mazoea” alisema Balozi Mapuri na kuongeza;

“Mnatakiwa kutambua kuwa mmeaminiwa na kuteuliwa kwa sababu ya imani ya Tume kuwa mnao uwezo wa kufanya kazi hii. Jambo muhimu mnalotakiwa kulizingatia ni kujiamini na kufanya kazi kwa weledi, na kwamba katika utendaji wa majukumu yenu mnapaswa kuzingatia Katiba ya Nchi, Sheria za Uchaguzi na kanuni zake, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Tume”

Kwa upande wake Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Mst) Thomas Mihayo akizungumza kwenye mafunzo ya watendaji wa Uchaguzi yaliyofanyika Mkoani Iringa aliwataka watendaji hao kuhakikisha kwamba wanayatambua na kuyajua vizuri maeneo ambayo uchaguzi utaendeshwa ikiwemo hali ya miundombinu ya kufika katika vituo vya kupigia kura.

“Mfanye utambuzi wa vituo vya kupigia kura mapema ili kubaini mahitaji maalum ya vituo husika kwa lengo la kuhakikisha mpangilio mzuri ambao utaruhusu uchaguzi kufanyika kwa utulivu na amani,” alisema Mhe. Mihayo na kuongeza;

“Niwasisitize kuhakikisha mnaajiri watendaji wa vituo wenye weledi wanaojitambua na kwa kadri inavyowezekana tuachane na undugu au upendeleo kwa ndugu na jamaa ambao hawana sifa za kufanya shughuli za uchaguzi” alisema.

Akizungumza kwenye mafunzo ya watendaji wa uchaguzi yaliyofanyika Mkoani Morogoro, Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mhe. Magdalena Rwebangira aliwataka watendaji hao kuhakikisha kwamba wanavishirikisha vyama vya siasa kwenye mchakato mzima wa uhaguzi huo.

"…..nawaasa kukumbuka kuvishirikisha Vyama vya Siasa na wadau wengine wa uchaguzi katika maeneo yenu katika masuala ya kiuchaguzi ambayo wanastahili kushirikishwa kwani jambo hilo litawarahisishia sana utekelezaji wa majukumu yenu," alisema Mhe. Rwebangira.

Aliwataka watendaji hao wa uchaguzi kuhakiki vifaa wanavyovipokea, kuhakikisha vinawafikia mapema wasimamizi wa vituo, kuhakikisha kila kituo cha kupigia kura kinafunguliwa saa 1:00 asubuhi siku ya kupiga kura na kufanya mawasiliano na Tume pale ambapo watahitaji ushauri kuhusiana na masuala ya uchaguzi.

Hivi karibuni Tume ilitangaza nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Amani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Tanzania Zanzibar na Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara ambapo kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyosainiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Dkt. Wilson Mahera Charles siku ya uchaguzi ilikuwa tarehe 17 Desemba, 2022.

Kata zilizotangazwa kufanya uchaguzi mdogo ni pamoja na Majohe iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dabalo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Ibanda iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mndumbwe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Njombe Mjini iliyopo Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Nyingine ni Misugusugu iliyopo Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Dunda iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mwamalili iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Mnyanjani iliyopo Halmashauri ya Jiji la Tanga, Lukozi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na Vibaoni iliyopo Halmashauri ya Mji wa Handeni.




# Makamishna wapya ECF SADC wapigwa msasa

***Na Mwandishi wetu***

Jumla ya Washiriki 60 wakiwemo Makamishna na Maafisa waandamizi wa Tume za Taifa za Uchaguzi kutoka nchi 9 wanachama zinazounda Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi za Kusini mwa Afrika (ECF – SADC) wamejengewa uwezo utakaowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, weledi, uwazi na uwajibikaji ili kuboresha uendeshaji wa uchaguzi kwa

Tume za Uchaguzi kutoka nchi wanachama.

Mafunzo hayo ya siku nne ambayo yalifanyika jijini Dar es salaam kuanzia tarehe 22 hadi 25 Novemba, 2022, yameandaliwa na Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi za Kusini mwa Afrika (ECF – SADC) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Taasisi ya Afrika inayojihusisha na ukuzaji wa Demokrasia (International IDEA).

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Mhe.Jacobs Mwambegele amesema vyombo vinavyosimamia uchaguzi vina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa michakato ya uchaguzi inaendeshwa katika mazingira ya uadilifu, uaminifu na uhalali.

Ili kufikia azma hiyo, Jaji Mwambegele amesema Tume za Uchaguzi zinapaswa kuzingatia kanuni na misingi ya uendeshaji wa uchaguzi kama vile kutoegemea upande, kutopendelea, uadilifu, uwazi, ufanisi na weledi.

"Ni matumaini yangu kuwa mafunzo haya yatachangia kuboresha uendeshaji wa uchaguzi katika nchi zetu na kuongeza uwezo wetu wa kusimamia uchaguzi," amesema.

Jaji Mwambegele ameongeza kuwa juhudi hizo zinalenga kuharakisha demokrasia endelevu katika ukanda na nchi zote wanachama kwa ujumla.

"Nakiri kuwa kabla ya kuteuliwa kwetu kwa nafasi mbalimbali katika Tume zetu za Uchaguzi tulikuwa watazamaji lakini sasa siyo watazamaji tena kwani jamii yetu inatutarajia tusimamie chaguzi zetu kwa uadilifu na weledi."

Washiriki wa mafunzo hayo ni Makamishna, na Maafisa Waandamizi wa Tume za Uchaguzi kutoka nchi za Botswana, Eswatini, Lesotho, Ushelisheli, Namibia, Malawi, Zambia, Zimbabwe na mwenyeji Tanzania.






# Tume za Uchaguzi zatakiwa kuboresha mwenendo wa uchaguzi

***Na Mwandishi wetu***

Tume za Uchaguzi kutoka nchi wanachama zinazounda Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (ECF SADC) zimeshauriwa kuhakikisha kuwa zinaboresha mwenendo wa uchaguzi katika nchi zao ili kuharakisha ukuaji wa demokrasia katika ukanda huo.

Akifunga mafunzo kwa Makamishna na Maafisa waandamizi wa Tume za Taifa za Uchaguzi kutoka nchi 9 wanachama zinazounda Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi za Kusini mwa Afrika (ECF –SADC), Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Dkt. John

Jingu amesema kuwa Tume za Uchaguzi zinapaswa kuongeza uwezo katika usimamizi wa uchaguzi pale zinapotekeleza majukumu yake.

Amesema uchaguzi ni nyenzo muhimu ya ulinzi na usalama katika nchi yoyote, hivyo washiriki hao hawana budi kuhakikisha wanaendesha uchaguzi unaoridhisha makundi yote ili kuepusha migogoro ya kiuchaguzi katika nchi zao.

Washiriki wa mafunzo hayo walijifunza kuhusu kuanzishwa kwa demokrasia na kanuni elekezi za usimamizi wa uchaguzi, viwango vya kimataifa vya uchaguzi na wajibu wa chaguzi za kidemokrasia, mwelekeo unaoibuka wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi na haki ya uchaguzi.

Washiriki wa mafunzo hayo wametoka katika tume tisa wanachama wa nchi zinazounda Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (ECF SADC) ambazo ni Botswana, Lesotho, Ushelisheli, Namibia, Malawi, Tanzania, Zambia, na Zimbabwe.

Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo yaliandaliwa mahsusi kwa ajili ya kuwatambulisha makamishna wapya wa uchaguzi na watendaji wakuu wa Vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi kuhusu dhana, kanuni elekezi, mienendo mizuri, na mielekeo inayoibuka katika nyanja ya usimamizi wa uchaguzi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo ambaye pia ni Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji wa Mahakama Kuu Mheshimiwa Asina Omari, pamoja na mambo mengine alisema mafunzo waliyopewa yana tija kwa kuwa yamewapa nyenzo za kutambua umuhimu wa tehama, matumizi ya mitandao ya kijamii, kushirikiana na wadau vikiwemo vyombo vya habari.





# Umoja wa Wanawake Wanasiasa watembelea Ofisi za Tume

***Na Mwandishi wetu***

Baadhi ya wanachama wa Jukwaa la Wanawake Wanasiasa nchini (TWCP-ULINGO) wametembelea Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo Njedengwa jijini Dodoma ili kutoa pole kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Raslimali watu wa ofisi hiyo, hayati Gerald Mwanilwa kilichotokea hivi karibuni.

Wanachama hao walilakiwa na Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Nassoro Shemzigwa ambaye aliambatana na Mkurugenzi wa

Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura, Bi. Giveness Aswile.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama wenzake, Mwakilishi wa jukwaa hilo, Bi. Saumu Rashid amesema wamefanya ziara hiyo kama wadau wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi lakini pia wamekuja kutoa pole kufuatia kifo cha hayati Gerald Mwanilwa ambaye enzi za uhai wake walifanya naye kazi sana hasa wakati wa Uchaguzi Mkuu uliopita.

“Tulikuja hapa kuhudhuria mkutano Mkuu wa wenzetu wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT), hivyo baada ya kumaliza mkutano ule sisi kama wadau tukaona tufike hapa, lakini pia tutoe pole kwenu kufuatia kifo cha mtumishi mwenzenu ambaye sisi tulifanya naye kazi sana hasa katika kipindi cha uchaguzi,” amesema Bi. Saumu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura, Bi. Giveness Aswile ambaye alizungumza kwa niaba ya uongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi aliwashukuru wanachama hao wa ULINGO kwa kuonesha upendo na kufika kuwafariji.

Pia Wanachama hao wa Jukwaa la Ulingo walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya ofisi za Tume pamoja na kukabidhiwa nakala ya ripoti ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

# SHAIRI

## Jitokeze Mwanamke, Ugombee Uongozi

***Na Mwandishi wetu***

Nashika yangu kalamu,kuhimiza wanawake
Nina jambo la muhimu, nawaomba mlishike,
Katika hii awamu, naomba msibweteke,
Kwa wingi jitokezeni, mgombee uongozi

Tathmini tukifanya ,tuone mmeshiriki,
Ushiriki ulo chanya,Majimbo muyamiliki,
Na kura kuzikusanya, kwa usawa pia haki,
Jitokeze mwanamke, ugombee uongozi,

Unganeni kwa pamoja,hamasa mkapeane,
Jengeni wenu umoja, na wala msitengane,
Kwani mkiwa wamoja ,mtayashinda mengine,
Hima mwanamke hima ,kagombee uongozi,

Mjue kujenga hoja , mkiwapo vikaoni,
Wingi wenu uwe hoja , mkae madarakani,
Msijefanywa daraja,wengine kuwapandeni,
Hima wanawake hima ,gombeeni uongozi,.

Tofauti mzizike, nguzo mama isimame,
Madaraka muyashike, kwenye kazi mjitume,
wala msijibweteke, mjitokeze kwa shime,
Mkipata uongozi ,malengo muyatimize,

Jueni yenu thamani, vyovyote vile iwavyo,
Muwe mnajiamini, msijefikiri sivyo,
Hakuna wa kuwahini,fanyeni mambo yalivyo,
Tokeni mkagombee, muyaongoze majimbo,

Ushindi mtaupata, bidii mkiongeza,
Taratibu mkifata , mtaweza kuongoza,
Na heshima mtapata, malengo mkitimiza,
Haya shime wanawake ,gombeeni uongozi

Nyie ndio ngao bora, walezi wa familia,
Walimu wenye ubora, mengi mnavumilia,
Mnazo njema bishara,Taifa kutumikia,
Hima mwanamke hima ,kagombee uongozi,

Twatambua mama zetu,majukumu mlo nayo,
Kuzilea koo zetu,nasi twawatia moyo,
Pamoja na dua zetu ,tuombe bila uchoyo,
Hima mwanamke hima ,kagombee uongozi.

Nimefika kaditama,usia nimemaliza,
Nawaomba kinamama,achene kwenu kuwaza,
Imara mkisimama, hakuna wa kuwatweza ,
Hima mwanamke hima , ugombee uongozi




Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania
Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV